

## HATUA ZA KUFUATA KABLA YA KUPATA KIBALI CHA UJENZI MANISPAA YA SONGEA

HATUA YA KWANZA: Andaa ramani ya nyumba utakayojenga, ramani unaweza kuipata kwa mtu yeyote anayechora ramani za nyumba kwa mfano anaweza kuwa Msanifu Ramani au Msanifu Majengo anaweza kukuchorea ramani nzuri.

HATUA YA PILI: Ramani inatakiwa kuidhinishwa na Msanifu wa Majengo aliyesajiriwa. Msanifu anaangalia ubora na vigezo muhimu vinavyotakiwa kwenye nyumba.

Likitokea tatizo kwenye nyumba Msanifu atawajibika kujibu ikiwa tatizo hilo litatokana na kosa la mchoro wa nyumba hiyo. Msanifu Majengo atapiga mhuri wake aliopewa na Bodi ya usajiri wa wasanifu majengo kwenye kila ukurasa wa ramani hiyo.

HATUA YA TATU: Kabidhi ramani hizo nakala nne kwenye ofisi ya Mkurugenzi ili zilipiwe ada ya kibali cha ujenzi na zisainiwe. Baada ya ramani kukabidhiwa wataalam wafuatao wanahitajika kuzikagua ramani hizo na kuzisaini 1. Afisa Ardhi, 2. Afisa Mipango Miji, Afisa Afya na Mhandisi wa Ujenzi.

AFISA ARDHI atakagua iwapo kiwanja kinamilikiwa kihalali na kinalipiwa kodi ndiyo maana inatakiwa kuambatanisha na Hati au Offer ya kumiliki kiwanja na risiti ya malipo ya kodi ya kiwanja ya hivi karibuni.

AFISA MIPANGO MIJI atakagua aina ya nyumba unayotaka kujenga na matumizi yake na atalinganisha kwenye ramani ya mipango miji ili ajue eneo unalotaka kujenga nyumba hiyo limepangiwa matumizi gani

AFISA AFYA:atakagua ukubwa wa madirisha na uhusiano wa matumizi ya chumba kimoja na kingine,pia atakagua shimo la maji taka.

HATUA YA NNE:Kutembelea kiwanja na kujiridhisha ili ajaze taarifa za kiwanja chako kwenye fomu hizo halafu atapiga mhuri wa ofisi ya ujenzi kama ishara ya kwamba kila kitu kipo vizuri.

HATUA YA TANO:Kuidhinishwa na Kamati Ndogo ya Mipango Miji ya Halmashauri husika.Ramani na fomu zote zitapelekwa kwenye kikao cha Kamati Ndogo ya Mipango Miji ambacho hukaa mara moja kila baada ya muda Fulani.

HATUA YA SITA:Kibali kutolewa,mar baada ya kikao cha Kamati ya Ujenzi kumalizika,vibali vyote vilivoidhinishwa hutolewa kwa wahusika.

Kinachotakiwa wakati wa mchakato wote huo,nakala nne za ramani ya nyumba ziwepo,ili mara baada ya kutolewa kibali cha ujenzi,nakala mbili zitabaki kwa mwenye nyumba na nakala moja itakwenda ofisi ya Ardhi na nakala moja itabaki Ofisi ya Ujenzi kama kumbukumbu.

Ukipata kibali chako unaweza kuendelea na ujenzi wako bila bughuza,kumbuka kutokuwa na kibali cha ujenzi

ukibainika unaweza kuzuiliwa kujenga(Stop Order) hadi hapo utakapopata kibali cha ujenzi.

KUMBUKA Sheria inamtaka kila mtu anayejenga nyumba kwenye eneo lililotangazwa kuwa la Mipango Miji awe na kibali cha ujenzi na asipokuwa na kibali hicho anaweza kuzuiliwa kujenga.

**Imetolewa na Albano Midelo**

**Afisa Habari Manispaa ya Songea**